Kujifunza Jinsi Ya Kufanyakazi Na Watoto Yatima Na Wale Walio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi

Mradi wa ushirikiano wa ustawi wa jamii kuhusu VVU/UKIMWI ushirikiano kwa ajili ya watoto yatima na waishio katika mazingira hatarishi zaidi Tanzania.

SIKU YA 7

Kuwasaidia watoto waishio na VVU/UKIMWI na watoto pamoja na familia zilizoathiriwa

Mchakato Wa Huduma Za Ustawi Wa Jamii Kwa Watoto Yatima Na Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Walioathiriwa Na VVU/UKIMWI.

1. Kuwafikia na kuwatambua
2. Kujenga uhusiano na watoto yatima na familia zao
3. Kutathmini mahitaji na uwezo wao
4. Kutengeneza mpango wa huduma: ambao ni pamoja na mitandao, utambuzi na kutoa rufaa kwenye vyanzo vingine vya huduma.

Mchakato Wa Huduma Za Ustawi Wa Jamii Kwa Watoto Yatima Na Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Na Walioathiriwa Na VVU/UKIMWI

5. Utekelezaji wa mpango wa huduma.
   - Tambua na toa rufaa kwa ajili ya rasilimali nyinginezo
   - Kutoa huduma za moja kwa moja Kutatua matatizo, kusaidia na kuratibu
   - Kuwawezesha na kuwasaidia walezi.
   - Shughulikia maswala ya kinga na huduma dhidi ya VVU.
6. Upimaji wa maendeleo, kurejea mpango wa huduma na ufuatiliaji kwa kupitia kesi menejimenti inayoendelea, Msaada wa familia na utetezi

Malengo

Kufikia mwisho wa siku Msaidizi ustawi wa jamii ataweza ku:

- Kuonyesha ufahamu kuhusu maswala ya msingi kuhusu maambukizi ya VVU/UKIMWI kuanzia maambukizi ya awali hadi mwishowa maisha.
- Kuelezea hali ya VVU nchini Tanzania, Kusini mwa jangwa la Sahara la Afrika na Dunia kwa ujumla.
- Kuonyesha ufahamu wa msingi kuhusu kinga dhidi ya VVU. Unasihi na upimaji Damu katika mtazamo wa Msaidizi ustawi wa jamii wa jamii

Malengo …

- Kuonyesha ufahamu wa msingi kuhusu kuzuia maambukizi ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto kuanzia wakati wa ujauzit, hadi kunyonyesha kwa mazingira ya Msaidizi ustawi wa jamii wa jamii
- Kuonyesha ufahamu kuhusu tiba ya VVU na stadi anazohitaji Msaidizi ustawi wa jamii kuwasaidia wanaoishi na VVU/UKIMWI kuzingatia tiba na kinga

Kweli Ya Msingi Kuhusu VVU Jinsi Vinavyoathiri Tanzania Na Dunia.

Maana Ya Neno HIV

.H Human (binaadamu) kwa sababu virusi vya UKIMWI vinamuathiri binadamu peke yake.

.I Immuno deficiency (upungufu wa kinga) unaosababishwa na VVU kudhoofisha kinga asilia ya mwili.

.V Virus kwa sababu vimelea hivi ni(virusi).Kwa tabia ya kirusi hakina uwezo wa kujizalisha chenyewe mpaka kiingie katika kiini cha celli mwilini mwa binaadamu.

7

Neno Ukimwi Lina Herufi Aambazo Zinawakilisha

U Upungufu (unaoptokea kwa sababu ya maambukizi) ni hali ambayo mtu hakuzaliwa nayo ila ameipata baada ya kuambukizwa.

U – Upungufu wa

KI Kinga– Kwa sababu huathiri mfumo wa kinga ya Asili unaodhibiti /kupambana na maambukizi ikiwemo vijidudu vya magonjwa kama virusi au bakteria

KI – Kinga

MWI Mwilini– Kwa sababu husababisha upungufu wa kinga kwa kudhoofisha mfumo wa kinga mwiliniHuvyo huruhusu magonjwa nyemelezi kumshambulia mtu ambae kinga yake ni dhaifu.

Mtu anayeugua UKIMWI kinga huwa dhaifu hivyo hukabiliwa na magonjwa mbalimbali nyemelezi yenye mkusanyiko wa dalili tofauti.

MWI – Mwilini

UKIMWI ni sehemu ya wigo wa maambukizi ya VVU unaoelezewa kuwa ni hatua ya mwisho ya ugonjwa.

8

VVU/UKIMWI – PIMA UFAHAMU WAKO		
Kweli	Si kweli	**Kondomu zinaweza kuzuia maambukuzi ya VVU.**
Kweli	Si kweli	**Dawa anazopewa mama mjamzito na mtoto anapozaliwa zinaweza kupunguza uwezekano wa kumuambukiza mtoto.**
Kweli	Si kweli	**Dawa za kudhibiti ongezeko la VVU huponya maambukizi yaVVU**
Kweli	Si kweli	**Dawa za kudhibiti ongezeko la VVU huweza kusitishwa kinga ya mgonjwa inapoimarika (CD4)**
Kweli	Si kweli	**VVU huweza kuambukizwa toka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa kujifungua.**
Kweli	Si kweli	**Unyonyeshaji wa maziwa ya mama ni kinga dhidi ya VVU kwa mtoto.**
Kweli	Si kweli	**Mwanaume mwenye VVU hawezi kujamiiana na mwanamke asiye na VVU kwa usalama.**
Kweli	Si kweli	**Ni salama kufanyakazi na, kula na au**

Zoezi

- Zungumza na jirani yako.
- Tengeneza orodha ya:
  - Njia ambazo VVU huambukizwa
  - Njia ambazo watu hufikiria UKIMWI unaweza kuambukizwa ambazo hazina ukweli(VVU haviwezi kuambukizwa kwa)

Njia Za Maambukizi Ya VVU Zilizo Zoeleka.

- Njia kuu ya maambukizi ni ngono isiyo salama.
- Toka kwa mama kwenda kwa mtoto
- Kuongezewa damu isiyosalama
- Kushirikiana vifaa vyenye ncha kali visivyo takaswa (vifaa vya kutogea, vya kufanyia tohara)

11

UKIMWI Hauwezi Kuambukizwa Kwa…

- Kushirikiana chakula na mtu mwenye VVU
- Kushirikiana choo
- Kushirikiana vifaa vya kulia chakula,vya kufanyia kazi, maji au taulo la kukausjia mikono
- Mahusiano ya kilasiku katika kuisha na mtu mwenye VVU
- Kufanyakazi pamoja na mtu mwenye VVU
- Kubusiana au kukumbatiana au kugusana na mtu mwenye VVU
- Kung'atwa na Mbu au kunguni

Hatua Za Maambukizi Ya VVU Na Mwendelezo Wa Kupungua Kwa Kinga– Dalili Zinaweza Kutokea Kwa Mwenye VVU Na Hutegemea Na Hali Ya Afya Ya Mtu Anayeishi Na VVU Kwa Ujumla Na Sababu Nyinginezo.

VVU/UKIMWI Hatua za mabadiliko

Kabla ya maambukizi | Maambukizi ya awali | Kuonekana kwa fingo mwili | Kipindi kisicho na dalili | matatizo ya ki afya kwa vipindi | Kuendelea kwa matatizo makubwa zaidi ya kiafya

Dawa dhidi ya VVU Hudhibiti kuendelea kwa matatizo.

progression

Hatua Za Kuendelea Kwa Ugonjwa: VVU/UKIMWI

MAAMBUKIZIYA VVU

DAWA DHIDI YA VVU

UKIMWI

Kupungua kwa celidamu zaCD4 Kadiri ugonjwa unavyoendelea, miaka10-12 baadae

1500 350 200 0

CD4 Celli damu (T Cells)

Maana Ya Maneno

- Wingi wa Virusi= kiasi cha virusi kadiri vinavyoongezeka kila siku
- CD4 celli damu au T Celli = celli damu za kinga zinazoharibiwa na VVU. Kiwango cha Kawaida cha CD4 ni 600 hadi 1500. kadiri ugonjwa unavyoendelea celli damu za CD4 hupungua hadi kufikia 0.
- Dawa dhidi ya VVU= Zina Mchnganyiko wa Dawa tatu toka katika makundi tofauti ya dawa,kawaida huwa katika kidonge kimoja.
- *Mlipuko*= Kutokea kwa ugonjwa kwa kiwango kikubwa kuliko kawaida
- *Mlipuko wa kuvuka mipaka ya nchi* = ni mlipuko wa magonjwa kwa upana zaidi unaovuka mipaka ya nchi moja na kuingia katika nchi nyingine duniani.
- *Magonjwa nyemelezi*= Magonjwa yanayotokea mara kinga ya mtu inapoathirika kama vile mtu mwenye VVU kinga huendelea kupungua na magonjwa nyemelezi humshambulia kwa sababu ya kudhoofika kwakinga yake. Kuna magonjwa takriban 29 yanayosemekana kuwa nyemelezi kwa wanaoishi na VVU/UKIMWI.

Matokeo Ya Mwendelezo Wa Ugonjwa.

- Katika hatua za mwanzo za maambukizi dalili huwa kama za homa ya mafua mara nyingine hakuna dalili zozote
- Kwa kawaida maambukizi ya VVU hayaonyeshi dalili zozote. Watu wenye VVU huonekana na kujisikia vizuri tu. Kipindi hiki huweza kuchukuwa muda mrefu.
- VVU huweza kuambukizwa toka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwengine ukiwa katika hatua yeyote ya ugonjwa. Isipokuwa tu hatua za tahadhari zikichukuliwa kabla ya maambukizi, au baada ya maambukizi

Mwendelezo Wa Ugonjwa…

- Ikiwa mtu atatibiwa kwa kutumia dawa za kudhibiti ongezeko la VVU kiwango cha kuambukiza hupungua kwa kiasi kikubwa.
- Ikiwa tiba yenye ufanisi itatumika, watu wenye VVU huweza kuishi maisha ya kawaida kwa muda mrefu na VVU huwa ni ugonjwa sugu kama ilivyo kisukari au pumu.
- Pasipo matibabu, VVU huendelea na kuingia katika hatua ya UKIMWI, Hali ya ugonjwa inayotishia uhai na uwezekano wa kuambukiza huongezeka.

Kiwango Cha VVU Pasipo Matibabu Idadi Ya Virusi Na Kuendelea Kwa Ugonjwa.

Hatua ya ugonjwa	Idadi ya virusi
Hakuna maambukizi	0
Hatua ya awali ya maambukizi	10,000,000
Kipindi cha ukimya- mwaka1-5	5,000
Kipindi cha ukimya- miaka 5-10	10,000
Hatua ya dalili za mwanzoni	100,000
mwendelezo kuelekea kwenye UKIMWI	1,000,000
mwendelezo kuelekea Kifo	10,000,000

Kiwango Cha VVU Baada Ya Matibabu

Hatua za ugonjwa	Viral Load
Hatua ya awali ya maambukizi	10,000,000
Kipindi cha ukimya- mwaka1-5	5,000
Kipindi cha ukimya- miaka 5-10	10,000
Hatua ya dalili za mwanzoni	100,000
Tiba yenye ufanisi dhidi ya VVU	50
Miaka kumi baadae ndani ya matibabu	50

VVU Hufanya Nini Mwilini?

- Magojwa maalumu yaitwayo magonjwa nyemelezi huweza kutokea mwilini.
- Mtu mwenye VVU ambaye amepata magonjwa nyemelezi anasemekana kuwa na UKIMWI.
- Mfano:
  - Kifua kikuu
  - Utandu mweupe mdomoni
  - Magonjwa ya ngozi
  - Saratani ya ngozi
  - Saratani zinazohusiana na VVU
- UKIMWI husemekana wakati CD-4 celli zinaposhuka chini ya 200 na huambatana na kupungua kwa uzito sana au kukonda na magojnwa nyemelezi.

Je UKIMWI Hufanya Nini Mwilini?

- Ni dalili zipi au magonjwa yapi hutokea?

Bungua Bongo

UKIMWI Hufanya Nini Mwilini?

- Homa za mara kwa mara zaidi ya mwezi mmoja
- Kupungua uzitochini ya 10% ndani ya mwezi mmoja
- Kuharisha kwa zaidi ya mwezi mmoja
- Kukohoa kwa zaidi ya mwezi mmoja
- Kutoka jasho usiku
- Malengelenge/mkanda wa jeshi(herpes zoster)
- Malengelenge sehemu za siri (herpes simplex II)
- Homa ya uti wa mgongo (Cryptococcal)
- Kuwashwa kwa ngozi
- Kupoteza kumbukumbu au tatizo la kufikiria vizuri
- Udhaifu usioweza kuelezeka, ganzi au maumivu, kichwa kuuma mfululizo, (dalili za mfumo wa fahamu)
- Saratani maalumu zinnazotekea kwa wenye UKIMWI
- Kuvimba kwa matezi mwili mzima(Generalized lymphadenopathy)
- Pneumocystic Pneumonia
- Homa ya mapafu/vichomi

Hali Halisi Ya VVU Ki-Ulimwengu Na Tanzania Kwa Sasa.

Mlipuko Wa VVU/UKIMWI-2009

Ulimwengu

- 2.6 millioni maambukizi mapya 2009
- 33.3 millioni wanaoishi na VVU ulimwenguni
- 1.8 millioni waliokufa kwa UKIMWI 2009
- 17 millioni Yatima watokanao na VVU/UKIMWI

Kusini mwa jangwa la Sahara- Afrika

- 22.5 millioni wanaoishi na VVU
- 1.8 millioni maambukizi mapya
- 1.3 millioni waliokufa kwa UKIMWI2009
- 90% ya watoto wenye maambukizi na wenye maambukizi mapya wanaishi kusini mwa jangwa la sahara - Afrika

VVU Na Umri Wa Kuishi Tanzania.

Mwaka 991, umri wa kuishi nchini Tanzania kwa wanawake ulikuwa miaka 54 na miaka 53 kwa wanaume

- Mwaka 2009 ***umri wa kuishi umefikia miaka 48 na UKIMWI unaongoza kuwa sababu ya vifo.***

Sources: Countryfacts Information Courtesy: CIA Worldbook, 2011; USAID. Sub-Sahara Africa. http://www.usaid.gov/locations/sub-saharan_africa/countries/tanzania/index.html **(downloaded July 20, 2011)**

Hali Ya VVU/UKIMWI Nchini Tanzania

- Watu millioni 1.4 wanakadiriwa kuwa wanaishi na VVU/UKIMWI mwaka 2009 nchini Tanzania.
- Kiwango cha maambukizi ya VVU kwa ujumla nchini Tanzania ni 5.7% ya watu wazima – Zidi ya mtu 1 kati ya 20 wana maambukizi ya VVU; Kiwango cha maambukizi kwa wanawake ni 6.6%. 4.6% kwa wanaume. Mijini kiwango cha maambukizi ni 8.7% (2008 Takwimu toka-Serikalini)
- Watoto 200,000 wenye umri 0 - 14 walikadiriwa kuwa wanaishi na VVU/UKIMWI (2009 Takwimu tola serikalini)

26

Sababu Za kijamii Zinazochangia Maambukizi Ya VVU/UKIMWI.

- ***Uchumi***
  - umasikini
  - Kufanywa kuwa mijini na kukosekana kwa msaada wa mtandao katika mazingira ya mijini
- ***Kijamii***
  - Wenza wengi unaojamiiana nao
  - Sumu ya pombe
  - Madawa na madawa ya kulevya
  - Utumikishwaji wa maswala ya ngono kwa wanawake
  - Unyanyapaa na uwazi
- ***Mila***
  - vurugu za kingono, kubakwa na utumikishwaji
  - Kuanza ngono mapema
  - Kurithi wajane

Maambukizi Ya VVU Tanzania

- ***Mambo yanayochangia***
  - Kuwa na wapenzi wengi
  - Kuanza ngono mapema
  - Kiwango kidogo cha matumizi ya kondomu
  - Kutofahamika kwa hali ya maambukizi ya VVU
  - Kukosa taarifa kuhusu afya ya maswala ua kujamiiana
  - Kiwango kikubwa cha maambukizi ya magonjwa ya ngono mengine.

Hatari Kubwa Kabisa Kwa Maambukizi Ya VVU

- Mwaka 2008, wanawake walikuwa zaidi ya asilimia 60 ya watu wanaoishi na VVU. Asilimia 75 ikiwa kwenye kundi la umri wa miaka 15-24.
- Wanawake walio katika ndoa hufanya ngono zisizo salama na wenza wao hata hivyo bado huwa katika hatari ya maambukizi.
- Kwa kusema ukweli njia kuu ya maambukizi ya VVU kwa wanawake Tanzania inaweza kuwa ni kwa kupitia kwa wenza wao ambao wan mahusiano ya kingono na watu wengine.

Chanzo : TACAIDS (2008, November) 'Tanzania HIV/AIDS and Malaria Indicator Survey 2007-2008

Kinga Ya Maswala Ya Ngono

Kumbuka:

Unapofanya ngono isiyosalama,VILE VILE unafanya ngono na wenza wote wa mwenza wako.

Kinga Ya VVU,Unasihi Na Upimaji.

Jinsi Ya Kujikinga Na VVU

- Acha kabisa
- **U**we mwaminifu
- **Tumia** kondomu
- Kawia kuanza ngono
- Zuia maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto
- Tibu magonjwa mengine ya ngono

Elimi kuhusu VVU inahitajika kwa hayo yote!

Mikakati Ya Kinga Ya Awali

- Kubadili Tabia

Tathmini Ya Hatari

- Je utajali ikiwa nitakuuliza baadhi ya maswali kuhusu afya yako? Hii itajumuisha afya yako ya maswala ya kujamiiana.
- Je umeanza kujamiiana –je una mahusiano ya kingono na mwanaume mwenzako au mwanamke? Ikiwa jibu ni ndio na wanawake, wanaume au wote?
- Je unachukua tahadhari ya magonjwa? Ikiwa jibu lako ni ndio elezea. Ikiwa sio kwanini?
- Je unatumia madawa yeyote ya kukustarehesha kwa kutumia sindano? Ikiwa jibu lako ni ndio je unashirikiana na watu sindano? Je unazisafishaje?
- Je una maswali yeyote ambayo ungependa kuniuliza
- Kuhusu afya ya maswala ya kujamiiana, UKIMWI au magonjwa ya ngono?

Source, Linsk, 2000

Mikakati Ya Kushughulikia Kinga Dhidi Ya VVU

- ***PUNGUZA UNYANYAPAA*** Unyanyapaa unaweza kujiingiza katika kupunguza tabia hatarishi
- Punguza matumizi ya pombe na madawa mengine yanayoathiri tabia za kawaida.
- Fahamu hali yako kuhusu VVU

Je upimaji wa hiari unasaidiaje watu?
Je upimaji wa hiari unawezaje kuunganisha na huduma?

Bungua Bongo

Upimaji Wa Hiari Wa VVU, Unasihi Na Upimaji.

- ***Upimaji wa hiari ni mwanzo muhimu wa huduma nyingine za VVU/UKIMWI zikiwemo:***
  - Kuzuia maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto
  - Kinga na tiba ya VVU na magonjwa yanayo ambatana pamoja na tiba ya kifua kikuu.
  - Msaada wa kisaikolojia na kisheria
  - Inawezesha rufaa ya mapema kwa ajili ya huduma na msaada ikiwemo upatikanaji wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI.

Upimaji Wa Hiari Kuhusu VVU

- ***Upimaji wa hiari mzuri na unasihi husaidia watu ku:***
  - Kujua hali zao kuhusu maambukizi ya VVU na kufanya maamuzi wakiwa na ufahamu.
  - Chunguza, tathmini na badili tabia hatarishi.
  - Wakabiliane vyema na hali zao kiafya
  - Huwezesha maisha channya zaidi na upange kwa ajili ya maisha ya baadae
  - Wasaidie watu wenye VVU kujikinga na kuwakinga wenzi wao pamoja na familia.
  - Wasaidie kujifunza vizuri kuwa wazi kuhusu hali zao katika mazingira yao ya kijamii na kimila.

38

Upimaji Wa Haraka Wa VVU

- ***Njia tunazotumia kwa sasa kupima:***
  - Damu toka kidoleni hufyonzwa kwenye kifaa chembmba kidogo au mate hupimwa kwa dakika 10.
  - Matokeo hupatikana kwa muda mfupi kama ilivyo kwa kipimo cha haraka cha mimba. Vilevile matokeo huthibitishwa kwa kipimo kingine kabla hayajatolewa rasmi.
  - Mbinu za kufanya ngono kwa usalama na kuunganishwa na sehemu za huduma ni lazima zijadiliwe pamoja na mnasihi.

Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Upimaji Damu Kwa Hiari.

- Wahamasishe watu wasiofahamu hali zao kupima, haswa wanawake walio katika umri wa kuzaa.
- Tengeneza utaratibu wa wenza kusaidiana (m.f. mume kumsaidia mke na watie moyo ili waishi maisha chanya.
- Wasaidie ili waweze kuzifikia huduma za upimaji (usafirishaji, msaada wa kundi rika,n.k.)
- Watie moyo ili wawe wazi kueleza matokeo ya vipimo na saidia mchakato wa mawasiliano kwa usalama na uwe chanya.

Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Upimaji Damu Kwa Hiari

- Wasaidie watu wakati wa mchakato wa upimaji na wakati wa kuwaelewesha matokeo ya vipimo.
- Hakikisha kuwa unasihi wa baada ya matokeo ya vipimo unatolewa kwa matokeo ya aina zote chanya au hasi.
- Saidia mchakato wa kubadili tabia kwa watu wanaojihusisha na tabia hatarishi kama:
  - Kuwa na wapenzi wengi unaojamiiana nao.
  - Kuanza ngono mapema
  - Tabia hatarishi za ngono
    - Ngono zisizo salama
    - Wanaume wanaofanya ngozo na wanaume wenzao.
  - Watumiaji wa madawa ya kulevya kwa kujidunga na madawa mengineyo yasiyoruhusiwa.

Msaada Kwa Familia Na Jamii Kuzuia Maambukizi Ya VVU Toka Kwa Mama Kwenda Kwa Mtoto.

Kweli Za Msingi Kuhusu Kuzuia Maambukizi Ya VVU Toka Kwa Mama Kwenda Kwa Mtoto

- VVU huambukizwa toka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa mchakato wa ujauzito, kujifungua na kunyonyesha.
- VVU wakati wa ujauzito vyaweza kupunguzwa kwa kiwango cha chini sana (<2%) kwa kumtibu mama mjamzito mapema iwezekanavyo.

Njia Za Maambukizi Toka Kwa Mama Kwenda Kwa Mtoto.



Mwongozo Mpya Wa Tiba Tanzania

1. Wakinamama wajawazito wote wenye VVU wanastahili kutumia dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI.
2. Tiba dhidi ya virusi (chini ya celli damu <350 CD4) Ni lazima waanze dawa mapema iwezekanavyo.
3. Wakinamama wote wajawazito wenye VVU na celli damu zaidi ya (>350 CD4) vilevile wanapaswa kuanza dawa mapema iwezekanavyo(utaratibu wa tiba unaweza kutofautiana)
4. Watotowaote waliozaliwa na wamama wenye VVU wanapaswa kunyonyeshwa kwa angalau miezi sita. Watoto wanaonyonyeshwa ni lazima wapate tiba ya kufubaza virusi kila siku kuanzia walipozaliwa hadi wiki 4 mpaka 6, au wiki1 baada ya kuacha kunyonya
5. Watoto wasionyonyeshwa wanapaswa wapewe dawa za kufubaza VVU hadi wanapoitimiza umri wa wiki 4 mpaka 6

Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamiikwa Wamama Wenye VVU

- Fahamu kweli kuhusu kuzuia maambukizi ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto
- Msaidizi ustawi wa jamii anaweza kusaidia wakinamama kuwakinga watoto wao na maambukizi
- Watie moyo wakinamama waanze matibabu
- Wape ushauri wakinamama ili waweze kupanga kuhusu kubeba mimba, kujifungua na kunyonyesha.
- Wasaidie wamama wenye VVU walio katika huduma, saidia familia zao kuwatia moyo kuhusu huduma.
- Toa taarifa kuhusu njia salama ya kumlishe mtoto na kumtunza.

Jukumu Ya Msaidizi Ustawi Wa Jamii:Ujauzito

- Fanyakazi pamoja na familia kuwasaidia wanawake wenye VVU, watoto wao na familia zao kwa ujumla.
- Wasaidie wakinamama kupanga ujauzito na kujifungua ili kupunguza maambukizi
- Waunganishe wamama wajawazito na watoa huduma za afya mapema iwezekanavyo.
- Wasaidie wamama wajawazito kufahamu hali zao kuhusu maambukizi ya VVU na kupata huduma wakatiwa ujauzito ikiwemo tiba za kufubaza Virusi kulingana na mwongozo.
- Wasaidie wamama wajawazito kupata msaada wa familia ili kupima afya zao, kupata huduma wakati wa ujauzito na huduma zinazohusu VVU.

Kuzuia Maambukizi Ya Mama Kwenda Kwa Mtoto: Wakati Wa Kujifungua

- Tiba dhidi ya VVU wakati wa kujifungua inaweza kuzuia maambukizi ya VVU kwenda kwa mtoto.
- Tiba hii ni lazima ifanyike katika vituo vya huduma za afya kama kliniki ya uzazi au hospitali.
- Wakinamama wanapaswa kufahamu hali zao kuhusu maambukizi ya VVU mapema iwezekanavyo.
- Tiba yenye ufanisi inaweza kupunguza maambukizi kwa kiwango kikubwa.

Jukumu la Msaidizi Ustawi Wa Jamii: Kujifungua

- Msaidizi ustawi wa jamii anapaswa kusaidia sawasawa na inavyokubalika na wataalamu wa huduma za afya kwa wamama wajawazito, wanaojifungua na wanaonyonyesha.
- Kusaidia familia,anapokabiliana na matatizo ya uzazi wa mtoto na anapopata matokeo ya VVU kwa pamoja. Mazingira mengi magumu ya familia yaweza kujitokeza wakati wa shinikizo kama huo.
- Wasaidiena wahudumu wa afya kuwasiliana maswala magumu ya ufahamu wa kitaalamu na mama pamoja na familia katika hali ambayo wote wataelewa kwa haraka.Muda ni muhimu sana.
- ***FIKIRIA DHARURA.***

Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii: Kujifungua

- Ufahamu kuhusu mwongozo wa kuzuia maambukizi ya mama kwa mtoto inahitajika ili kusaidia wakinamama waelewe yale ambayo Daktari anawaeleza.
- ***Msaada unajumuisha sababaau mbalimbali kama vile:***
  - Kuandaa usafiri kwa wakati
  - Upimaji na muongozo wa tiba inayokubalika dhidi ya VVU
  - Kushinda vikwazo vinavyozuia kujifungulia hospitali.

Fanya Maamuzi Ya Au Kunyonyesha Au Kumpa Maziwa Kwa Chupa Ya Kunyonyea Kwa Wamama Wenye VVU

- Katika miezi miwili ya mwanzo, mtoto anayenyonya kwa chupa yuko katika hatari ya kifo kwa kuharisha, magonjwa ya njia ya hewa au magonjwa mengine mara 6 zaidi ukilinganisha na mtoto anayenyonya ziwa la mama yake.
- Hii ni mara nyingi kwa sababu maji yasiyosalama hutumika katika kuchanganyia maziwa ya unga ,chupa hazina usafi wa kutosha matumizi ya chupa si salama au maziwa yanayochanganywa ni kidogo kuliko mahitaji halisi ya ukuwaji wa mtoto.
- Kubadili kati ya maziwa ya mama na maziwa ya chupa huongeza uwezekano wa magonjwa

Kufanya Maamuzi Ya Au Kunyonyesha Au Kumpa Mtoto Maziwa Ya Chupa Kwa Mama Mwenye VVU

- Taratibu za kimila husaidia unyonyeshaji.
- Ikiwa watoto hawanyonyeshwi, watu watahoji hali yako kuhusu VVU na inawaweka wote hatarini mama na mtoto kutengwa au kunyanyapaliwa kwa namna nyingine.
- Kunyonyesha maziwa ya mama tu pasipo kumpa mtoto kitu kingine kwa miezi 6 ya mwanzo isipokuwa tu kama lishe mbadala ina:
  - Kubalika
  - Wezekana
  - Gharama inawezekana
  - Endelevu
  - Ni salama

Muongozo Wa Unyonyeshaji Kwa Wakinamama Wenye VVU

Mahali ambapo maziwa ya mama ni chaguo bora la kumlisha mtoto:

Nyonyesha maziwa ya mama kbila ya kumpa kitu kingine chochote kwa miezi 6 ya mwanzo tu, kisha

- Muanzishie vyakula vingine mbadala na uendelee kunyonyesha kwa miezi1***2***. Likiza taratibu kisha endelea kutibu kwa angalau wiki 1 baada ya kuachana na maziwa ya mama.
  - ***Ifikapo miezi 6***, endelea kunyonyesha pamoja na vyakula vingine vya ziada ikiwa vigezo vina:**Kubalika,Wezekana,Gharama inawezekana, ni Endelevu na Ni salama** havitafikiwa. Likiza kwa kipindi kuanzia siku 2−3 mpaka wiki 2−3 **.**

Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Kufanya Maamuzi Ya Kunyonyesha

- Msaidie mama pamoja na familia kuelewa kweli kuhusu kunyonyesha kwa wenye VVU.
- Hakikisha kuwa mama anaelewa utaratibu unaohitajika kwa unyonyeshaji salama, ikiwemo tiba ya VVU kwake mwenyewe na mtoto.
- Wasaidie wakinamama wapate huduma za afya kwa matatizo ya matiti, pamoja na vidonda au utando mweupe kinywani mwa mtoto.
- Isaidie familia kuelewa umuhimu wa shughuli za ulishaji salama kwa wamama wenye VVU.

Dawa Za VVU/UKIMWI Kuzifikia Huduma Za Afya Magonjwa Mengine Yenye Uhusiano Na VVU.

Tiba ya VVU: Kweli Za Msingi Kwa Msaidizi Ustawi Wa Jamii

- VVU vinatibika lakini haviponi
- Tiba ya VVU inahitaji angalau mchanganyiko wa dawa tatu humezwa kwa pamoja
- Madhara madogo madogo yanaweza kutibika kwa kusaidiana na watoa huduma za afya.
- Ikiwa dawa za VVU hazikuzingatiwa kwa angalau kiwango cha 90-95%, VVU Vitajenga usugu na tiba haitaweza kuwa na ufanisi mzuri.
- Pindi watu wanapoanza tiba dhidi ya VVU, Hawapaswi kuacha kwani watahatarisha afya na yao pamoja na ya wengine.

Lengo La Matibabu Dhidi Ya VVU

1. Kupunguza idadi ya VVU mwilini kufikia kiwango ambacho hakiwezi kuonekana kwa vipimo tulivyonavyo,chini ya (<50/ mm^3)
2. Rejesha na au hifadhi utendaji wa kinga
3. Boresha hali ya maisha
4. Punguza magonjwa yanayohusiana na VVU.
5. Punguza usugu wa dawa wakati virusi vinapojibadlisha hivyo kundi ladawa kuwa sugu na haziwezi kutibu tena.
6. Zuia magonjwa nyemelezi kwa kutumia dawa aina mbalimbali zinnazoweza kuchangia afya njema na kuimarisha uhai.

Masuala Ya Matibabu Dhidi Ya VVU

1. Madhara mengi huisha baada ya wiki chache Ikiwa hayatakwisha ni muhimu kuonana na mtoa huduma za afya.
2. Dawa ni kwa maisha yote, Isipokuwa tu kama kuna madhara makubwa yaliyojitokeza, m.f. kuathirika kwa mfumo wa fahamu.
3. Dawa dhidi ya VVU zinahitaji mlo kamili ambao kimsingi wengi wa waTanzania hawana uwezo wa kuupata.
4. Hii inaweza kujumuisha vidonge vingi na taratibu za kumeza ni mgumu kiasi.

Usugu Wa VVU Kwenye Dawa

- Usugu unamaana kuwa VVU haviwezi tena kutibika na dawa ambayo hapo awali ilikuwa ikiwatibu.
- Usugu kwa ujumla unauhusiano na kutozingatia dawa.
  - Ikiwa mtu hatazingatia tiba dhidi ya VVU
  - Ikiwa mtu amepoteza uwezo wa kufikia huduma ya matibabu kwa sababu ya miundombinu au vikwazo vya muundo vilivyopo.
- Watu wengine wanaweza kuambukizwa Virusi sugu kupitia ngono isiyo salama au tabia hatarishi nyinginezo au toka kwa mama kwenda kwa mtoto.
- Ni vigumu zaidi na ni ghali sana kutibu mgonjwa mwenye virusi sugu

Kuzingatia Tiba Maana

Kuzingatia: maana yake ni kufanya umezaji wa dawa za VVU kwa muda sahihi, kwa kiasi sahihi angalau kwa 90-95 asilimia ya muda

Kuto kuzingatia tiba: kunaweza kujumuisha kukosa kunywa dawa, kunywa dawa kwa kidogo kuliko kipimo halisi, kunywa dawa zaidi ya dozi halisi kunywa dawa wakati anapojisikia kuumwa tu n.k.

Utumiaji Wa Dawa Za Kufubaza VVU

- Kupima utayari wa kuzingatia dawa (kufuatilia matibabukwa ujumla)
- Upatikanaji wa dawa na huduma za afya
- Kutoa msaada katika kutumia dawa
- Kutengeneza mpango wa kuhakikisha ufuatiliaji
- Maswala ya kuwa wazi kuhusu hali ya maambukizi.
- Kutambua na kuendeleza mafanikio.
- Utambuzi wa matatizo.

Kupima Utayari Wa Kuzingatia Matibabu

- Je matibabu yako sahihi kama inavyotakiwa kiafya?
- Je mgonjwa yuko tayari kuendelea kumeza dawa?
- Je mlengwa ataweza kunywa dawa kwa usahihi (90-95% ya muda)?

Je tunawezaje kusaidia kwa ufanisi kuzingatia matibabu ya dawa dhidi ya VVU?

Vipi Kuhusu Kukosa Kunywa Dawa?

- Je jambo hili hutokea kwa wateja wako?
- Je hukutokea unapokuwa kwenye matibabu?
- Je watu wako tayari kukiri kuwa wamekosa kunywa dawa?
- Je kunamadhara gani yatakayotokea kwa kukosa kunywa dawa?
  - Halisi
  - Yanayo hofiwa

Kokosa Kunywa Dawa…

- Je unajisikiaje unapokosa kunywa dawa?
- Je hii ni?
  - Kosa au kasoro?
  - Ni jambo la kawaida linaloweza kumtokeakila mtu.
  - Ni jambo la kuchukiza na la aibu
  - Mengineyo?
- Je kukosa kitu, unapoteza kitu au kusahau kitu kuna maana gani katika mila na desturi zawatanzania?
- Je kuwa na kasoro au kufanya kosa kuna maana gani katika mila maalumu zawatu?

64

Kubadili Kukosa Kunywa Dawa

- Kukosa kunywa dawa humtokea kila mtu.(kuifanya hali ya kawaida)
- Kukosa kunywa dawa kunapaswa kutusaidia kujifunza jinsi ya kuepuka jambo hjli siku za mbele.
- Kukosa dozi moja kwa kawaida hakutasababisha matatizo
- Kumwambia mtoa huduma kuhusu kukosa kumeza dawa ili kwa namna ujisaidie wewe mwenyewwe kina Wengine.

65

Ni Lipi Jukiumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Kusaidia Umezaji Dawa Kwa Watu Wenye VVU?

Bungua Bongo

Ni Lipi Jukiumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Kusaidia Umezaji Dawa Kwa Watu Wenye VVU …

- Kumsaidia mtu mwenye VVU kufanya maamuzi kama wako tayari kuanza kumeza dawa
- Kuwasaidia kujiwekea utaratibu wa kumeza dawa kila siku.
- Kuwasaidia kuzifikia huduma ikiwemo tiba na kupata nyongeza ya dawa zinapokaribia kuisha.
- Msaidie mlengwa na familia kutatua matatizo ya mtu binafsi, familia au matatizo ya kijamii yanayohusu matatizo ya utumiaji dawa.

Ni Lipi Jukiumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Kusaidia Umezaji Dawa Kwa Watu Wenye VVU …

- Tetea swala la kuzifikia huduma na tiba.
- Mawasiliano kati ya Msaidizi ustawi wa jamii na watoa huduma za afya. Mtu anayeishi na VVU,Familia na jamii kwa ujumla.
- Msaidie mtu anayeishi na VVU kuelewe kuwa afya yake kwa ujumla ni ya muhimu kama ilivyo kuzingatia matumizi ya dawa kwa kila siku.

Ni Lipi Jukiumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Kusaidia Umezaji Dawa Kwa Watu Wenye VVU …

- Msaidie mtu mwenye VVU kuelewa umuhimu wa lishe na kutatua matatizo kuhusu usalama wa chakula.
- Msaidie mtu mwenye VVU kuelewa kuwa uvutajinsigara, unywaji wa pombe, matumizi ya madawa mengine na kujihusisha kwa hali ya juu katika maasuala ya ngono ni kinyume na utaratibu wa tiba.
- Msaidie mtu anayeishi na VVU kutatua maswala ya kiutawala kama vile jinsi gani ya kuendeleza kwa kiwango chenye mwendelezo wa upatikanaji wa dawa za kufubaza VVU kulingana na utaratibu uliopo wa tiba.

Ni Lipi Jukiumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Kusaidia Umezaji Dawa Kwa Watu Wenye VVU…

- ***Msaidie mteja kuelewa namna ya kuzingatia dawa dhidi ya VVU na jinsi ya kufanya hivyo.***
  - Msaada wa familia
  - Msaada wa mfumo wa afya.
  - Kusaidia katika matibabu na kutibu madhara yanayojitokeza ili kuzuia kutozingatia.
  - Matibabu yanayoendelea, elimu na msaada.

Lipi Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Kusaidia Kuzingatia Taratibu Wanazopewa Na Watoa Huduma Za Afya?

- Kumsaidia mtoa huduma kuelewa hali ya kisaikolojia ya mgonjwa
- Kumsaidia mtoa huduma kuelewa ufahamu kuhusu Huduma za VVU na tiba kwa mtazamo wa mgonjwa.
- Kumsaidia mtoa huduma kuielewa familia, jamii na mfumo wa kijamii wa kusaidia matibabu na kuzingatia.
  - lugha, umbali, upatikanaji wa huduma, mila kuhusu huduma.
- Kumsaidia mtoa huduma kutatua migogoro mingine, madhara ya dawa, na uchovu wa tiba

Jinsi Gani Msaidizi Ustawi Wa Jamii Anvyosaidia Familia Zenye Watoto Wanaoishi Na VVU

- Wasaidie watoto kuelewa kuwa wanamaisha ya baadae marefu na mazuri ikiwa watazingatia matibabu kwa usahihi.
- Saidia kupata rasilimali zinazohitajika
  - Msaada wa fedha
  - Makazi na lishe
  - Elimu
  - Usafirishaji
  - Upatikanaji wa huduma za afya
- Toa elimu juu ya VVU kuongeza uelewa wa jinsi ya kutoa msaada na kupunguza unyanyapaa.
- Ratibu huduma zinazohitajika na rufaa.

Kushughulikia Magonjwa Mengine Yanayoambatana Na VVU(Matatizo Yaliyoambatana

- Mchanganyiko wa magonjwa ikiwemo kifua-kikuu, malaria na homa ya ini inahitaji
- Magonjwa ya ngono yanapaswa kutibiwa
- Magonjwa nyemelezi ni magonjwa ambayo watu wenye VVU huyapata kwa sababu ya kudhoofika kwa mfumo wa kinga.
- Magonjwa nyemelezi yanaweza kuzuilika na kuugua na vifo kupungua kwa kiwango kikubwa kwa kutumia dawa ambazo ni za kawaida , zinzopatikana kirahisi na kwa bei nafuu.
- Hata hivyo watu wenye VVU wanahitaji huduma yenye mwendelezo ili kupata huduma hizi za tiba.

Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii Kwa Magonjwa Mengine

- ***Saidia upatikanaji*** wa uelewa wa na uhusiano wa huduma zinazoendelea kuhusu VVU.
- Hakikisha kuwa Watu wanaoishi na VVU hupata huduma za uchunguzi wa afya zao wa mara kwa mara zenye mwendelezo.
- Saidia mabadiliko yanayohitajika katika mila na hakikisha huduma za afya zinaendelea kwa watu wenye VVU.
- Huduma endelevu kwa wenye VVU.

Kila Msaidizi Ustawi Wa Jamii Anapaswa Kufahamu kuhusu Kuwakinga Watu Wenye VVU.

Kweli Za Msingi Kuhusu Kujikinga Kwa Watu Wanaoishi Na VVU

Kuwakinga wanoishi na VVU kuna maana gani kwa wenye virusi, hupunguza uwezekanowa wa maambukizi mapya, kupunguza tabia hatarishi kuhakikisha kwamba hawawaambukizi watu wengine.

Watu wanaoishi na VVU wanaweza kufanya ngono, lakini mara zote inapaswa iwe salama kwa kutumia kinga

- Matibabu yenye ufanisi ya VVU hupunguza Mzigo wa virusi kwa mwenye VVU.Lakini pamoja na matibabu yenye ufanisi ni lazima kondom itumike ili kujikinga mwenyewe na yule unaye jamiiana naye.

Kweli Za Msingi: Kinga Kwa Wagonjwa Wenye VVU

- Tiba dhidi ya VVU yenye ufanisi ni njia mojawapo bora zaidi inayowezekana kupunguza maambukizi mapya kwa sababu kiwango kidogo sana cha virusi kisichoweza kupimi inamaanisha ya kwamba mgonjwa ana uwezekano mkubwa wa kuto ambukiza VVU kwa watu wengine.
- Watu wenye maambukizi wanapaswa kuwa na uhakika kuwa hawatumii sindano zilizotumika au kujihusisha katika shighuli zitakazo sababisha maambukizi kwa njia ya damu.

Kweli Za Msingi: Kinga Kwa Wenye VVU

- Hupunguza hatari ya maambukizi ya VVU.
- Hupunguza maambukizi mapya ya aina nyingine ya virusi.
- Inapunguza uwezekano wa kupata maambukizi ya magonjwa ya ngono
- Hupunguza maambukizi yatokanayo na damu, m.f. Homa ya ini. (Hepatitis)
- Inaongeza wigo wa kuaminiana na upendo kati ya wenza wenye hali ya maambukizi inayotofautiana
- Inapunguza msongo, inafanya mahusiano ya kingono na tabia zinazoambatana kuwa ya kawaida

Muhtasari: Mamboya Muhimu Kwa Msaidizi Ustawi Wa Jamii Kusisitiza Kwa Wenye VVU

- Tiba ya VVU inakabiliwa na uhaba wa rasilimali ambazo inabidi zitunzwe na kuheshimiwa.
- Mara dawa za kufubaza VVU zinapoanza kutumika ni lazima ziendelee kutumika kwa maisha yote.
- Ni lazima dawa zote zimezwe kama ilivyo shauriwa na mtoa huduma.
- Tiba ya VVU humuathiri mwenye VVU,familia yake na wengine wanao toa msaada.
- Wanaoishi na VVU ni lazima wafahamu kuwa wanapaswa wajadili kila jambo ikiwemo tiba za nyumbani ambazo mgonjwa amepewa na Daktari ili kuwe na uhakika kuwa hakuna madhara yeyote ya mwingiliano wa madawa

Muhtasari: Mamboya Muhimu Kwa Msaidizi Ustawi Wa Jamii Kusisitiza Kwa Wenye VVU…

- Madhara yatokanayo na tiba ya VVU nilazima yashughulikiwe kwa tahadhari kuzuia usumbufu wakati wa kumeza madawa.
- Kuzingatia kumeza dawa za muda mrefu kunahitaji msaada binafsi wa kijamii ambao hubadilika kila baada ya muda.
- Kinga kwa wenye VVU ita saidia kudumisha ufanisi wa dawa zinazo tumika kwa sasa kudhibiti VVU.
- Kuzingatia kunahitaji utetezi wa jamii na taifa kwa ajili ya upatikanaji wa huduma.
- 100% ya watu wenye VVU wanapaswa kupewa matibabu kwa ufanisi. Haswa wananwake walio katika umri wa kuzaa,watoto na vijana.

Athari za VVU Kwa Muda Mrefu:

Kuwa muwazi,Mjadala,Mpango wa mwisho wa Uhai.

Kweli Za Msingi: VVU Na Athari Za Muda Mrefu

- Ikiwa tiba imefanyika vizuri kwa kutumia dawa zenye ufanisi mapema iwezekanavyo ili kulinda utendaji kazi wa kinga ya mwili, watu wanao ishi na VVU wanaweza kuishi muda wa kawaida wa uhai wa binadamu
- Tiba dhidi ya VVU inahitaji upatikanaji wa uhakika kwa muda wote wa dawa,huduma za afya na upimaji na msaada unaohitajika kwa magonjwa sugu ya muda mrefu ikiwemo upatikanaji wa moja kwa moja wa dawa za kufubaza VVU, ukaribu , msaada wa kisaikolojia na msaada wa kijamii.

Athari Za VVU Za Muda Mrefu HIV Maambukizi Na Tiba Ndani Ya Familia

- Msaada wa familia kwa anayeishi na vvu unahitajika kumsaidia watu waishio na VVU Ili kuendeleza tiba , mazingita anatakiwa kufafanua jambo.
- Familia yenye wazazai ambao wanaishi na VVU Inaweza kukabiliana na unyanyapaa kama ilivyo kwa mwenye VVU mwenyewe. Familia zinazo nyanyapaliwa zinahitaji msaada wa kisaikolojia na elimu kuhusu VVU.
- Japokuwa mwanafamilia anatibiwa, hatimae tiba inaweza kuwa sio yenye ufanisi, kuongeza msaada wa huduma na mzigo wa kihisia katika familia..

VVU: Mwelekeo Ramani Ya Njia Kueleke Kwenye Tanzania Bila VVU

Je Msaidizi Ustawi Wa Aamii Ana Mchango Gani Katika Kuwezesha Tanzania Kuwa Na Kizazi Kisicho Na UKIMWI?

- Msaada kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi na familia zao.
- Msaada kwa aji li ya upimaji na tiba.
- KANYAGA/TUPILIA MBALI UNYANYAPAA
- Saidia kuelimisha jamii na familia.
- Unda , Endeleza, Saidia na tanua

KANYAGA/TUPILIAMBALI UNYANYAPAA– SAIDIA JAMII NGUVU YA KUMI

Ramani Ya Njia Kuelekea Tanzaniaa Bila VVU

Matibabu
•Tibu wattoto wote wenye maambukizi Kwa asilimia100. upatikanaji wa huduma za kuzuia maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto (PMTCT+)
•Tiba kwa asilimia100. ya watu Wanaokidhi vigezo vya kuanza dawae. Endeleza uzingatiaji mzuri wa dawa.
•Tibu magonjwa yaliyoambatana kama kifua kikuu, magonjwa ya ngono.

Kinga ya Awali
• Acha kabisa ngono
• Kuwa mwaminifu
• Tumia Kondom
• Tohara kwa wanaume
• Chelewa kuanza kufanya ngono
• Tibu magonjwa ya ngono kwa ufasaha
• Pima mapema na mara kwa mara
•Wasaidie watoto waishio katika mazingira hatarishi,wanawake na familia
•Waelimishe wanaume, wananwake na vijana.
•Ondoa kabisa utumikishwaji wa wanawake
• ubakaji(Kinga baada ya uwezekano wa maambukizi) → PEP
• Biashara ya ngono
• Ndoa za mapema

Kinga kwa wenye VVU
Ngono salama
Punguza idadi ya watu unao fanya nao ngono
Kuzuia maambukizi ya mamakwenda kwa mtoto
•Tunasubiri dawa za kuua wadudu kwa wakina mama (microbicides)
•Tunasubiri kinga kable ya maambukizi ya VVU (PrEP)

Sehemu Zenye Taarifa Muhimu Kuhusu VVU

- www.globalhealth.org
- www.avert.org
- www.iasusa.org
- www.thebody.com
- www.aidsportal.org
- Aids.gov
- Aidsinfo.nih.gov
- www.cdc.gov/hiv
- www.nigeriahivinfo.com
- Usaid.gov/our_work_global_health/aids/countries/Nigeria.html

Muongozo wa kuzuia maambukizi ya VVU toka kwa mamakwenda kwa mtoto umebadilika, Jan 2011
Kwa maelezo zaidi angalia katika mtandao Shirika la Afya Duniani. (WHO)

http://www.who.int/pmtct
http://www.who.int/child_adolescent_health/doc

Mafunzo Ya Kuwajengea Stadi Day 7
Mpango Wa Huduma Wakati VVU Ndio Swala La Kulishughulikia

- Chagua mwandishi wa kumbukumbu atakaye wasilisha kazi kesho asubuhi wakati wa kutoa mrejesho.

Jadili mashaka, maswali toka mada tulizojifunza leo ikiwemo:

  - Nia mbadala za unyonyeshji wa mtoto badala ya ziwa la mama mwenye VVU
- Jadili mahitaji yanayohusiana VVU kwa mtoto na familia katika kisa cha kikundi chako.
- Fanya kazi katika vikundi vidogo.
  - Fanya mahojiano na mteja,au mwana familia kuhusu hatari ya maabukizi ya VVU au mahitaji.
  - Wasaidie kutengeneza mpango ili wapime afya zao au wapate huduma.
- Mjadala katika kundi kubwa. Je mmejifunza nini?